**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# TAARIFA YA SPIKA KUHUSU KUONGEZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UFUATILIAJI NA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MIPANGO YA MAENDELEO YA TAIFA

Ofisi ya Bunge,
10 Barabara ya Morogoro,
S.L.P. 941,
40490 Tambukareli
**DODOMA.**

Septemba, 2026

**Waheshimiwa Wabunge,**

Siku ya Jumatatu tarehe 31 Agosti, 2026 Kamati ya Uongozi ilikutana, kujadili na kuamua kuhusu uhitaji wa Bunge kuunda Kamati kwa ajili ya kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Dira na mipango ya Maendeleo ya Taifa. Uundaji huo ulitokana na utafiti uliobaini kwa sasa tunafanya uchambuzi na kujadili mapendekezo ya Mpango na si utekelezaji wake. Kamati ya Bajeti ikishapitia mapendekezo ya Mpango, ufuatiliaji hufanyika kwa ngazi ya kisekta.

Utaratibu huo umeonekana kuwa na upungufu ambao suluhisho lake ni kuanzisha Kamati mpya ya Bunge. Kamati hiyo itakuwa mahsusi kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mipango ya Taifa kwa ngazi ya kitaifa na kwa muktadha mtambuka.

Kama mnavyofahamu Kamati ya Uongozi ndiyo yenye jukumu la kushauri kuhusu uendeshaji bora wa Shughuli za Bunge kama ilivyofafanuliwa katika Fasili ya 2(3) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025.

Aidha, baada ya Kamati ya Uongozi kushauri kuhusu uhitaji wa kuanzisha Kamati hiyo mpya, niliitisha Kikao cha Kamati ya Kanuni ili niweze kushauriana nayo kuhusu suala hilo kwa mujibu wa Fasili ya 3(3)(b) na (d) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni. Baada ya majadiliano, Kamati ilishauri Bunge kuunda Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ufuatiliaji na Tathmini ya

Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa. Ushauri huo wa Kamati ni kwa mujibu wa Kanuni ya 179(3) ya Kanuni za Bunge.

**Waheshimiwa Wabunge,**

Kamati hii itaongozwa na Naibu Spika. Wajumbe wa Kamati watakuwa ni wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge. Kwa ujumla Kamati hii itakuwa na jukumu la kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Dira ya Taifa na Mipango ya Maendeleo ya Taifa. Msingi wa majukumu ya Kamati ni Taarifa za Tume ya Taifa ya Mipango kuhusu Ufuatiliaji na Tathmini ya Mipango ya Taifa. Kwa mantiki hiyo majukumu yake hayataingiliana na majukumu ya Kamati nyingine.

Kwa hali hiyo Kamati ya Kanuni ilipitisha marekebisho ya Kanuni katika Nyongeza ya Nane kwa kuiongeza Kamati ya Ufuatiliaji na Tathmini kuwa moja ya Kamati za Kudumu za Bunge za Sekta Mtambuka.

Marekebisho hayo ya Nyongeza ya Nane yamewasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili aweze kutangaza katika Gazeti la Serikali kwa mujibu wa Kanuni ya 180(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Baada ya hatua hiyo kukamilika, tutachapisha na kugawa kwa Wabunge nakala za vitabu vipya vya Kanuni.

Mussa Azzan Zungu (MB)
**SPIKA WA BUNGE**